

Kampeini husaidia kueneza ufahamu

MULIKA TB MALIZA TB

Mulika TB! Maliza TB! ni kampeini kabambe inaendeshwa kitaifa ili kuimarisha ufahamu kuhusu Kifua Kikuu na idadi ya watu waliopimwa hadi maradhi hayo yatakapokomesha. Ishara ya mienge ilitolewa kwa kaunti 10 zilizoathirika zaidi kote Kenya ili kuashirikia kujitolea kwa serikali na washikadau wake katika harakati za kukomesha Kifua Kikuu.

Jifunze zaidi

<http://nltp.co.ke/the-mulika-tb-maliza-tb-concept>
au Mulika Maliza kwenye mtandao wa Facebook.



PAZA SAUTI KULIKO KIFUA KIKUU ni kampeini ya kimataifa iliyoanzishwa na Muungano dhidi ya maradhi hayo, ukiwaleta pamoja washirika wa kibinafsi na wa umma kuhamasisha wananchi na kupaza sauti kuhusu maradhi haya yanayoua. Mashirika arubauni yanajumuika katika kampeini hii ya **#LouderThanTB**, ikiwa ni pamoja na UNITAID, UNICEF, WHO, Médecins sans Frontières, Save the Children, Stop TB Partnership, na mengine mengi. Huduma yake ni kuleta ufahamu kuhusu maradhi ya Kifua Kikuu katika watoto na kutafuta njia bora za kuwatibu watoto.

Jifunze mengi kuhusu 'Paaza Sauti Kuliko Kifua Kikuu kutoka kwa **TB.org**, au tafuta **#LouderThanTB** kwenye mtandao wa Facebook, Twitter, au Instagram.



MULIKA TB
MALIZA TB



TB ALLIANCE

REPUBLIC OF KENYA



MINISTRY OF HEALTH

Je ni kikohozi tu?

Jinsi ya kumkinga
mtoto wako dhidi ya
Kifua Kikuu.



#ChildTBmeds



TB ALLIANCE

Kifua Kikuu ni nini?

Kifua Kikuu ni maambukizi katika mapafu ambayo yanaweza kusababisha ugonjwa. Watu wengi huonyesha dalili za ugonjwa huo, lakini kwa wengine wengi zaidi, Kifua kikuu hujificha na huenda ikalipuka baadaye. Kifua kikuu husambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kupitia hewa hasa wakati mtu anakohoa au kupiga chafya. Mtoto wako anapovuta hewa yenye viini, huenda akaugua Kifua Kikuu.

Mtu yeyote anaweza kuugua Kifua Kikuu. Kila mwaka, maelfu ya watoto nchini Kenya huambukizwa Kifua Kikuu na wengi wao hufariki. Mtoto wako pia anaweza kuugua maradhi hayo anapovuta hewa yenye viini. **Hata hivyo, kuna habari njema:** Mtoto wako anaweza kutibiwa na kupona iwapo utampeleka apimwe.

Dalili unazopaswa kuchunguza



Kikohozi



Kupunguza uzito



Homa au kutokwa na jasho usiku



Kuwashwa-washwa na kupunguza michezo

Watoto wanaweza kuugua Kifua Kikuu nyumbani, shuleni au mahala kokote ambapo watoto hukaa sana. Mtoto wako pia anaweza kuambukizwa Kifua Kikuu, ikiwa wewe, mtu mwingine yoyote katika nyumba, kazini au shuleni anaugua maradhi hayo. Baadhi ya watoto wanaouguua Kifua kikuu huonekana wagonjwa lakini wengine hawaonyeshi dalili yoyote. Ikiwa hauna uhakika, njia bora zaidi ya kumkinga mtoto wako ni kumpeleka afanyiwe ukaguzi.

Maradhi ya KIFUA KIKUU yanaweza kutibiwa

Kile unachopaswa kufanya

Sasa kuna dawa iliyotengenezwa hususani kwa ajili ya watoto. Dawa hii ni tembe ambayo huyeyuka ndani ya maji na ina ladha ya matunda. Hivyo basi ni rahisi kwa mhudumu kumpa mtoto kwa urahisi.

Tiba ya Kifua Kikuu inapatikana katika vituo vyote vya afya vya serikali bila malipo.

Ikiwa wewe au mtu yeyote katika nyumba, kazini au shuleni anaugua Kifua Kikuu, mtoto wako pia anaweza kuambukizwa.

Baadhi ya watoto wanaouguua Kifua Kikuu huonekana kuwa wagonjwa lakini wengine hawaonyeshi dalili zozote. Ikiwa hauna uhakika, njia bora zaidi ya kumkinga mtoto wako ni kumpeleka afanyiwe ukaguzi kwenye kituo cha afya.

Tiba ya Kifua Kikuu inapatikana katika vituo vyote vya afya vya serikali bila malipo.

Iwapo unaugua Kifua Kikuu au kuonyesha dalili zozote za ugonjwa huo, basi peleka watoto wako kwa kituo chochote cha afya kilichoko karibu ili wapimwe. Kuwapeleka wapimwe kutahakikisha wanapata matibabu na kuponywa iwapo pia wanaugua Kifua Kikuu.

Kuna zaidi ya vituo vya afya 4,000 vinavyotoa huduma za matibabu ya Kifua Kikuu hapa nchini Kenya.

Kile unachopaswa kukumbuka



Kuna dawa na matibabu ya Maradhi ya Kifua Kikuu



Mtu yeyote anaweza kuugua Kifua Kikuu; hata watoto wamo hatarini



Iwapo mtoto wako, au mtu yeyote anayekaa naye anaonyesha dalili za maradhi hayo, mpeleke mtoto wako apimwe



Hapa nchini Kenya madawa ya watoto yanapatikana sasa



Hakikisha umemaliza tiba ili uondoe viini vyote vya maradhi ya Kifua Kikuu. Kwa njia hii unaepuka kupata maradhi hayo tena



Kaa chonjo - mpeleke mtoto wako katika kituo cha afya